# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu :**

**Mkuu wa Shule: 0754 360 615**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0673 532 794/0678929332**

**Malezi: 0675057209**

**Shule ya Sekondari Florian**

**S.L.P 279 KARATU - ARUSHA**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI FLORIAN HALMASHAURI YA KARATU MKOA ARUSHA MWAKA ................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ............. na atasoma tahasusi ya CBA/CBG/HGL

Shule ya Sekondari **Florian** ipo umbali wa Kilometa 21 Kusini mwa Mji wa Karatu. Usafiri wa gari kutoka mjini Karatu unapatikana katika kituo cha mabasi Karatu Nauli ni Shilingi 4,000/= kwa gari na shillingi 15,000/= kwa pikipiki au bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ................ Mwisho wa kuripoti ni tarehe ....................

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi dark blue mshono “V” mbele, iwe ndefu ifike juu kidogo ya kisigino, jozi mbili.
ii. Mashati meupe ya mikono mirefu jozi mbili.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iv. Sare ya Michezo ni tracksuit dark blue yenye mistari meupe pembeni jozi moja
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;viatu vyenye shingo ndefu(buti) havitaruhusiwa.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
vii. Sweta dark blue yenye mshono wa V shingoni.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) sketi mbili rangi ya damu ya mzee marindaya kawaida ya kupanga, jozi mbili.
ix. Tai dark blue yenye mistari meupe
x. T-shirt mbili zenye nembo ya shule (1 Orange na 1 Kijivu, zenye kola ambazo hujulikana kama ”form six” ) zinapatikana karibu na shule kwa anayehitaji kwa gharama ya Tsh. 14,000/= kila moja

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter book 3 Quire mbili kwa kila somo
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Oxford advanced learner dictionary kwa wanafunzi wa HGL
v. Scientific Calculator
vi. Godoro la futi mbili na nusu kwa sita

vii. Mashuka ya pink Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha
ix. Vyombo vya chakula viwe ya alluminium (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
xi. Panga 1, Brush ndogo ya chooni 1 yenye kopo lake, na Rubber squeeze 1 kwa wanafunzi wa CBG na HGL
xii. Jembe 1, Hard broom 1 na soft broom 1 kwa wanafunzi wa CBA
xiii. Dissecting kit/ board/tray kwa wanafunzi wa CBG na CBA, aje na kimojawapo.
xiv. Spring file 1
xv. Lab coat kwa wanafunzi wa michepuo ya CBA na CBG.
xvi. Taa ya mwanga wa jua (Solata). Zingatia ya mwanga wa jua.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha taslim hazipokelewi shuleni hivyo malipo yote yafanyike kupitia account ya shule yenye jina **FLORIAN SEC. SCHOOL** kupitia account namba **40901200042** iliyoko katika benki ya NMB na pay-in-slip kuwasilishwa kwa mhasibu wa shule siku ya kuripoti.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na

utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Namba za simu za wazazi/walezi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………

Jina la Mkuu wa Shule ……………………………………

Mhuri wa Mkuu wa Shule **………………………………....**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: 0754360615
- Makamu Mkuu wa Shule: 0673 532 794/0678929332
- Mwandamizi Taaluma: 0767162135
- Mwandamizi Malezi: 00675057209

# FLORIAN SECONDARY SCHOOL

E-mail: floriansecondaryschool@gmail.com
Website: www.floriansecondary.ac.tz

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

To be completed by Medical Officer in a Government Hospital.

Full Student's Name: ……………………………………………………………………………………………………………………….

Age: ……………………………………………………………………….Sex: ……………………………………………………………

1. "AIDS" Test …………………………………………………………………………………………………………………………
2. Blood count (Red & White) ………………………………………………………………………………………………
3. Urine examination ……………………………………………………………………………………………………………..
4. Stool examination ……………………………………………………………………………………………………………..
5. Syphilis Test …………………………………………………………………………………………………………………………….
6. T.B. Test ……………………………………………………………………………………………………………………………….
7. Ear Test ………………………………………………………………………………………………………………………………..
8. Eye Test ……………………………………………………………………………………………………………………………….
9. Abdomen ……………………………………………………………………………………………………………………………..
10. Spleen ……………………………………………………………………………………………………………………………………
11. UTP………………………………………………………………………………………………………………………………………
12. Additional information or any other physical mental hereditary or infections diseases:
    ………………………………………………………………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………………………………………
    (Please state nature of treatment)

    Medical Certificate:
    I certify that the above mentioned has been examined and found it to/ no to pursue further education.
    Signature……………………………………………………………….
    Designation ………………………………………………………….
    Station …………………………………………………………………
    Date ………………………………………………………………………………….. Official stamp……………………………………..

SHULE YA SEKONDARI FLORIAN

TAARIFA NA MKATABAWA UTII KWA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

1. TAARIFA (HISTORIA) YA MWANAFUNZI
    a) Jina la mwanafunzi……………………………………………
       Jinsia(me/ke)………………….umri……………………………
       Mtaa/kijiji anapoishi…………………………………………..

    b) Jina la mzazi/mlezi……………………………………………
       Mji/kijiji/mtaa anapoishi……………………………………….
       Mawasiliano ya mzazi/mlezi
           Simu ya mkononi……………………….
       Au………………………(baba/mama)
       …………………………………………………….
2. MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI SHULENI

   Mimi…………………………………………………naahidi kwamba sitashiriki migomo ya aina yeyote shuleni,sitafanya fujo zozoteshuleni wala kutenda kosa lolote la jinai na nakubalikutii sheria,kanuni na taratibu na maelekezo yote nitakayopewa katika muda wote nitakapokuwa shuleni.

   Jina la mwanafunzi…………………………………………
   Sahihi……………………………
   Tarehe…………………………..

3. KUKIRI KWA MZAZI KUTOA USHIRIKIANO

   Mimi…………………………………………….ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………………….nakiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule wakati wote atakapokuwa anasoma

   Jina…………………………………………………….
   Sahihi………………………………………………….
   Tarehe…………………………………………………..

   NB fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni.

